**Kila mtu ana malaika (03) - Mimba zisizotakikana**
Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

**Wahusika:**

Annie
Angela
Anita
Ma Tily
Jet
Leyla
Pinto

**Utangulizi:**

Karibuni katika Jifunze kwa Kusikia, Mlango wa tatu wa mlolongo wa mchezo wetu wa kuigiza wenye sehemu 10 na ulio na jina la Malaika wa Kila Mtu, Tunayafuatiliza maisha ya vijana wetu wanapowasiliana wenyewe kwa wenyewe pale wanapokuwa katika umri wa kubaleghe.

Angela ni mja mzito, aliye na mimba ya miezi saba, na hajamuelezea yeyote shuleni juu ya kisa hicho. Sasa amebaki peke yake, huku akikabiliwa na masuali mengi yasiokuwa na majibu.

Annie anafika nyumbani kwa Angela kutaka kujuwa kwanini Angela alisikia kichefuchefu darasani.

Hebu tuungane nao katika Mlango wa tatu wa Kisa cha Malaika wa Kila Mtu.

**Onyesho la Kwanza: Jikoni**

| | |
|---|---|
| SFX | Radio inasikika/ Sahani zinakoshwa |
| ANNIE: | (anazima muziki) Hodi Hodi! Kuna mtu yeyote nyumbani humu? |
| SFX | Mlango wa jikoni unafunguka/unafungika |
| ANGELA: | (amehuzunika) Ingia Annie |
| ANNIE: | Karibu hapa. Hebu nikumbatie Shoga. |
| SFX | Busu na mminyo |
| ANNIE: | Jee mama yako yuko? |
| SFX | Sahani zinaondoshwa |
| ANGELA: | Hata, atakuja punde hivi. |
| ANNIE: | Wacha kujishughulisha, Angela. Kaa chini. Umekuwa ukilia. Mimi niliingiwa na wasiwasi jana pale ulipoondoka darasani namna ile. Unaumwa? |
| ANGELA: | Si mgonjwa, Annie (Bubuta) (Nong’ona). Nina mimba. |

| | |
|---|---|
| ANNIE: | (apigwa na butaa) Nini? Angela. Unasema nini, wewe? Siamini. Una hakika? Imekuwaje? |
| ANGELA: | Angalia. Shati langu limekuwa likiificha mimba hiyo. Anaglia? |
| ANNIE: | Mola Wangu Eee - Nani, vipi imekuwa? Wewe hutoki nje? Sijawahi kukuona katika Party? |
| ANGELA: | Binamu wangu walinialika hapo kwa jirani. (Akibubujika machozi) Ahhh Annie. Kwa nini mimi? Sijawahi kulala na mtu ye yote hapo kabla, sijawahi, hiyo ilikuwa mara moja tu. Naweza kufa. Mama amekasirika kweli. Amempigia simu mjomba Billy kumwambia amuarifu Pinto. |
| ANNIE: | Pinto? |
| ANGELA: | Hilo ni jina la utani la yule mvulana, mlango wa jirani. Nitajiuwa! |
| SFX | Mlango wa jikoni unafunguka/ unafungika |
| ANNIE: | Maselebi, hujambo? Nilikuwa niondoke punde hivi. (Ananong'ona). Kwa heri shoga. Changamka. Tutazungumza baadae. |
| SFX | (Kwa sauti kubwa zaidi) Mlango unafunguka/ ungafungwa. |
| ANITA: | Angela. Wacha kulia. Rafiki yako ana jukumu. Lazima abebe dhamana kwako. Huwezi kubakia nyumbani kwangu. Punde pale ndugu yangu atakapopiga simu na kuniambia nambari ya simu ya huyo kijana na anwani yake, basi utakusanya mabegi yako na kwenda zako. |
| MUZIKI | unaanza kusikika. |

**Onyesho la Pili: katika nyumba ya Ma Tilly**

| | |
|---|---|
| SFX | Sauti ya TV iko juu. |
| ANNIE: | (Juu ya TV) Maa. |
| MA TILLY: | Nini? Siwezi kusikia. |
| ANNIE: | Maa, kwa hisani yako punguza TV. |
| MA TILLY: | Nini? Siwezi kusikia. Ninaangalia TV. |
| ANNIE: | (akipiga kelele) Nitakwenda kusafisha nyumba ya Gogo Nati. |
| MA TILLY: | (anapunguza sauti ya TV) Haina haja ya kupiga kelele. Mimi si kiziwi. Unaelekea wapi? |
| ANNIE: | Nyumbani kwa Gogo Nati. Kufagia kidogo. |
| MA TILLY: | Time nyingi sasa, ama sivyo? |
| ANNIE: | Bwana , haitochukuwa muda mrefu |

MA TILLY: Ah, ni saa Kumi na Mbili na Nusu, inaanza. Nenda zako. Sitaki kukosa mwanzo.
ANNIE: Baadae nitakwenda kwa Angela kucheza muziki.
MA TILLY: Shh sasa
ANNIE: Kwa heri maa
SFX Hamna jibu: Sauti ya TV yapandishwa juu.

**Onyesho la tatu: jioni mapema**

SFX Crickets. Mlio juu ya mlango wa chuma.
ANNIE: Jet! Ni mimi.
JET: (kutoka ndani, sauti iliyochoka) Sawa, ninakuja sasa hivi.
SFX Mlango unafunguka.
JET: (Akisinzia) Ndio kwanza natoka kwenye majenzi kule mjini
ANNIE: Kwa nini kiza hivi?
JET: Nilifikiri ungependa kupunga hewa kidogo, hapa. Nitawasha taa.
SFX Kijiti cha kibiriti kinawashwa, kunanuka herufu ya mafuta ya taa.
JET: Imekuwaje: Jamani - Kwa nini umenuna?
ANNIE: (amechukia) Mama yangu hajali. Kile anachokijali ni kutizama michezo yake ya kuigiza jioni.
JET: (anacheka) Sawa, kwa hivyo tunaweza kufurahia zaidi.

ANNIE: Jee mimi sio muhimu kuliko televisheni yake? Hajali wapi nilipo au nini ninachofanya.
JET: Angalia - Ninajali. Unataka kujuwa vipi?
ANNIE: (Bado kakasirika) Vipi?
JET: Nimebakisha nguo zangu kwa ajili yako. Wewe maisha unaifanya kazi hiyo vizuri. Baadae utaweza kujinunulia kitu kizuri kutokana na fedha utakazopata. Ama sivyo? Maji yashapata moto jikoni, kwa hivyo mshukuru Mola, changamka.
ANNIE: Hmmmm sawa.
JET: Njoo - Bado ninataka kulala. Kuna wakati mwingi bado. Njoo (akibusu) njoo hapa.
SFX Kitanda kinalia. Anabusu
JET: Umeshameza tembe za kujizuwia usipate mimba?
ANNIE: Ndio - Unanijuwa mimi!
JET: (Akibusu) Hmmm - Nakuuliza tu.

ANNIE: Na badae lazima niende kwa Angela. Yeye ni shahidi wangu.

**Onyesho la nne: Sebuleni**

SFX Muziki unacheza. Unamalizika.
ANNIE: Na sasa? Ungependa kusikiliza kitu kingine?
ANGELA: (Mwenye furaha) Lilikuwa jambo zuri. Ahsante kwa kuja.
ANNIE: Ilikuwa vigumu kwa mimi kujitenga na Jet, lakini nikwambie kweli wewe ni muhimu zaidi.
ANGELA: (Mwenye huzuni) Annie, kitanitokea nini?
ANNIE: Kwanza kabisa, wewe utapata mtoto na sisi sote tutakusaidia.
ANGELA: Maa hatafanya.- Ananichukia. Ananifukuza.
ANNIE: Hata kidogo, Angela. Hakuchukii, ila tu ana hasira. Atatulia. Nisikilize - nipe mkono wako. U baridi sana, maskini kipenzi changu. Nafikiri unahitaji kunielezea hadithi nzima. Kile ninachokijuwa ni kwamba ulikwenda kwenye party pamoja na Layla na Mo. Na sasa huyu Pinto. Nini kimetokea, hebu niambie. Itakusaidia pindi utasema.
ANGELA: Naam. Ilikuwa jumamosi, mwezi wa Septemba uliopita. Maa alitaka kumtembelea rafiki na hajataka kuniacha peke yake. Haniamini, hiyo ndio shida. Hajawahi kuniamini.
SFX Kiunganisho cha muziki. Sauti za harakati katika party.
ANGELA: Ilikuwa Party. Tulikunywa pombe kidogo. Tulikutana na hawa vijana - Steve na Pinto. Walivutia sana. Pinto ndiye aliyezungumza sana.
PINTO: Nyiye Wasichana. Mnafanya nini?
LAYLA/ANGELA: Poa tu. (akicheka)
PINTO: Karibu. Chukuwa nyingine!
SFX Mkebe wa biya unafunguliwa. Sauti ya kumwagika.
PINTO: Kuna Party nyumba ya jirani.
ANGELA: Lakini nilifikiri unaishi hapa.
PINTO: Ndio. Nyumba ya Steve iko kule. Ana chakula na muziki poa. Njoo! Poa tu!
SFX: Anacheka. Anashawishika.
ANGELA: Hakuna Party hapa.
LAYLA: Tutarejea Angie. Jee unakuja?
PINTO: Hatakuja.
ANGELA: Si - si sasa hivi Layla. Nitaungana nawe baadae.
PINTO: Njoo, kaa hapa. Jina lako?

| | |
|---|---|
| SFX | Sauti ya kubusu. Mvuto mkubwa wa pumzi. |
| SFX | Kiunganisho cha muziki. |
| ANNIE: | Ulikuwa sio salama Angela, hasa ulikuwa ulivyokuwa umelewa. Ulevi unakutoa akili. |
| ANGELA: | Nilijihisi salama kabisa - Nilisisimka - nikiwa mikononi mwake. Nilijihisi na furaha. Nilitaka kubakia hivyo maisha. Ilikuwa mara yangu ya kwanza na Pinto alikuwa mwema kwangu. Ni tafauti kabisa na vile nilivyotarajia. Mama alielezea kama kitu cha kuchukiza na kichafu, lakini hajaelezea kitu chochote vizuri. |
| ANNIE: | Mama yangu pia. Wanafikiri tu kwamba sisi tunajuwa, kwa kuangalia TV au sinema. Lakini wao walijuwa kwa kutenda. Hata hivyo, nilibahatika. Lazima ilikuwa si wakati mzuri wa mwezi. Pale alipojuwa kwamba situmii dawa, alishikilia kwamba niende kliniki kuchunguzwa. Tangu wakati huo nimekuwa nikidondwa sindano mara hadi mara. Niko salama. |
| ANGELA: | Huyo kijana ni nani? |
| ANNIE: | Yule kijana aliyoko katika kituo cha taxi |
| ANGELA: | Nimefurahi kwamba mapumziko ya shule yameanza. Itabidi niamke mapema niende kiliniki kesho. |
| ANNIE: | (amestaajabu) Ah?(Mpigo) Nafikiri kutoka sasa unahitaji kuchunguzwa kila wakati. |
| ANGELA: | Hiyo pia. Sio. Daktari alinichunguza damu. |
| ANNIE: | Kachunguza damu? |
| ANGELA: | Naam. Alisema kitu. Kwa hakika sijafahamu. Alichukuwa damu kidogo. Alisema huo ni uchunguzi wa HIV. Nitapata  matokeo kesho. Annie. Na hofu sana. Ina maana gani? Jee nitakufa? (Mshindo wa kilio) |
| ANNIE: | Sio, bila ya shaka sio. Shhhhh. Nitakwenda pamoja nawe (kwa upole) Shhhh. Tutafahamu tukiwa pamoja. Usijitie wasiwasi kwa sasa. |

**Hitimisho:**

Malaika wa kila mtu ni mchezo wa kuigiza ulioandikwa na Romie Singh. Na ni hayo kutoka Jifunze kwa kusikia kwa leo. Kwa hisani  yako jiunge nasi tena mara nyingine na ujuwe kama Sugar Daddy ya Annie ni kweli mtamu hivyo?. Jee, rafiki yake, Djamila anaweza kumsaidia Angela pale anapojitahidi kuelewa nini maana ya uchunguzi wa HIV, una maana gani hasa? Kumbuka, ikiwa unataka kukisikiliza kipindi hiki tena au kuwaarifu marafiki juu yake, basi fungua Website yetu www.dw-world.de/lbe Kwa herini.